



“UKIDANGA UTADANGWA”

UTANGULIZI

Kudanga ni aina ya mahusiano ya ngono baina ya mwanamke na mwanamme kwa ajili ya kupata pesa, zawadi au hadhi. Kudanga ni tabia inayoshamiri na kujengeka miongoni mwa vijana wenye umri kati ya miaka 15-24 ambao pia kwa kiasi kikubwa wanakabiliwa na changamoto ya kupata maambukizo mapya ya VVU.

Wataalamu wanatafsiri tabia hii kuwa ni matokeo ya umasikini pamoja na tabia za utegemezi,

mfano wasichana kutegemea wanaume au wavulana kutegemea wanawake.

Vyovyote itakavyokuwa, ushahidi wa kitafiti unaonesha kuwa tabia ya kudanga ina mchango mkubwa katika kuwaweka vijana katika hatari ya kupata VVU na maradhi mengine ya kujamiiana.

SABABU KUU ZA KUDANGA

- Vijana hujiingiza kwa sababu za kupandisha hadhi zao katika jamii mfano kuwa na mahusiano na watu maarufu (kupata kiki).

- Kutaka kumiliki vitu vya thamani ambavyo hawana uwezo navyo kama simu, gari na kutaka kuendana na mabadiliko ya maisha.
- Kuwa na kiwango kidogo cha Elimu ya Afya ya Uzazi, VVU na stadi za maisha.
- Kupata ushawishi kutoka kwa marafiki na vijana rika.
- Kutumia vibaya mitandao ya kijamii
- Kukosa ajira na umasikini.

MADHARA YA KUDANGA

- Kudanga kunaongeza uwezekano wa vijana kupata maradhi ya kujamiiana ikiwemo VVU, homa ya ini na saratani ya mlango wa shingo ya kizazi.
- Wasichana wanaoshiriki tabia za kudanga zinawaweka katika

hatari kubwa ya kujiingiza katika biashara ya ukahaba (Sex work) kama tabia hiyo itakuwa ni tegemezi au itafanywa kwa muda mrefu.

- Kupata mimba zisizotarajiwa na zile za umri mdogo.
- Kushindwa kutimiza ndoto na malengo ya maisha uliyojiwekea.
- Kupoteza heshima yako, familia na jamii.

NJIA ZA KUEPUKA KUDANGA

- Epuka marafiki na vikundi viovu/hatarishi
- Tafuta njia za halali za kujipatia kipato kuondosha utegemezi
- Jenga uthubutu, jiamini, jithamini na sema **“hapana”**
- Shiriki michezo yenye tija
- Fanya ibada

UNAWENZA KUAMBUKIZWA VVU KWA KUDANGA. BADILIKA!

Kimetayarishwa na **TUME YA UKIMWI ZANZIBAR**



Simu: ++255 24 223 5694, Barua pepe: info@zac.or.tz

[f Tume ya Ukimwi Zanzibar](#) [Zanzibar_aids_commission](#) [Tume ya Ukimwi Zanzibar](#) www.zac.or.tz